HISTORIA YA PAROKIA YA BMC - KIGAMBONI

Parokia ya Bikira Maria Consolata, Kigamboni ilizaliwa kutoka Parokia ya Mt. Yosefu katika mchakato ufuatao:

Kati ya miaka 1939 – 1942, Wakatekumeni kadhaa walipata ubatizo katika parokia ya Mt. Yosefu, wakristu hao waliongezeka polepole ambapo kufikia mwaka 1960 tayari kulikuwa na jumuiya kubwa yenye kaya Zaidi ya waumini 30 wakisali chini ya mti wa mzambarau (wakati huo) kwenye eneo la shule ya msingi Kigamboni.

Mwaka 1969, Mkuu wa shirika la wamisionari waconsolata Padre Liyori alileta ombi kwa Mhashamu Baba Askofu Edger Marantha wa Jimbo la Dar es salaam wakati huo, juu ya kuanzisha utume wa wamisionari waconsolata eneo la Kigamboni. Baba alikubali ombi hilo.

Mwaka 1970, Ujenzi wa kanisa na nyumba ya Mapadre ulianza na kukamilika mapema mwaka 1973. ujenzi huo ulifanywa na jumuiya ya waamini chini ya usimamizi wa mapadre wa Consolata, chini ya Padre Orsola ambaye alikua Paroko wa kwanza wa parokia hii na msaidizi wake Padre Julio, Imc.

Baada ya kuanzishwa, Parokia ya Bikira Maria Consolata iliendelea kukua, na waumini kuongezeka. Moja ya ishara za kukua ni pamoja na kuanzishwa kwa vigango na Parokia teule ambazo nazo vilikua na kuwa Parokia kamili. Ifuatayo ni orodha ya Parokia na parokia teule zilizozaliwa kutoka Parokia ya BMC:

i. Parokia ya ya Wat. Anastazia na Florian, Kimbaji,
ii. Parokia ya Mwenyeheri Yosefu Allamano, Kibadada,
iii. Parokia ya Mt. Marko Muinjili, Mjimwema,
iv. Parokia ya Mt. Paulo VI, Mikwambe,
v. Parokia ya Bikira Maria ya Consolata Nyota ya Asubuhi, Geza Olole,
vi. Parokia ya Bikira Maria Mama wa Mungu, Vijibweni.
vii. Parokia ya Mwongozo

Hadi sasa, Parokia ya Bikira Maria Consolata haina kigango ama Parokia iliyo chini yake. Hata hivyo, idadi ya waumini imeendelea kuongezeka ambapo kwa sensa ya waumini yam waka 2024/2025, jumla ya waumini takribani elfu tatu (3,000) wanahudumiwa kwenye parokia ya BMC.

Kuanzia mwaka 1973 hadi 2023 Parokia imefanikiwa kukuza na kulea miito mitakatifu ya ndoa, upadre na utawa kwa watoto na vijana. Upande wa wito wa upadre, tunamshukuru Mungu kwa zawadi ya wito kwa mapadre watano na shemasi mmoja wazao wa Parokia yetu:

1. Pd. Beno Kikudo,
2. Pd. Novatus MBaula,
3. Pd. Edwin Mwakigomba,
4. Pd.Raymond Mbaula,
5. Pd. Gonzaga Gonza Haule (Mbenedictine).
6. Pd. Nicolaus Paskal Nkoronko
7. PD. Englibert Kilasala

Kutoka Jumuiya moja ya kwanza mwaka 1960 iliyokuwa na kaya zaidi ya 30, sasa tunazo Jumuiya 59 (yenye kaya 1,400) ambazo zinafanya kazi chini ya hierakia na Halmashauri ya walei kamati tendaji ya parokia.
Kutokana na jumuiya hizo sasa tuna kanda 4 zenye jumla ya jumuiya 59 kama ifuatavyo:

1. Kanda ya kivukoni: Jnn 9,
2. Kanda ya Tuamoyo: Jmy 13,
3. Kanda ya Kisiwani: Jnn 13,
4. Kanda ya Tungi Jnn 24.

Matukio muhimu ya Parokia ya BMC ni pamoja na uadhimishaji wa Jubilei ya miaka 50 iliyofanyika mwaka 2023.
Shughuli zilizofanyika kama sehemu ya tukio hili kuu ni kama ifuatavyo:

1. **Kuwasha mshumaa**: Jubilei ya miaka 50 ya Parokia yetu ilifunguliwa mnamo tarehe 18 juni 2022 katika adhimisho la Misa Takatifu iliongozwa na pd. Vincent Mpwaji, katibu jimbo kwa tukio la kuwasha mshuma ambao umeendelea kuwaka hadi sasa, kuzindua salamu ya jubilee na sala la Jubilei.
2. **Semina ya Familia**: kwa lengo la kukuza roho ya utume wa familia pamoja na kujali uhai. Kukoleza na kujenga imani ya waamini. Kutambua familia kama chuo cha upendo na sala.
3. **Matenembezi ya kimisionari**: Katika parokia ya manda-Dodoma tukiwa na lengo la kuenzi kazi iliofanywa na wamisionari, kujenga urafiki baina parokia hizo mbili, kubadilishana uzoefukatika utume tukitambua kwamba umisionari ni wajibu wa kila mbatizwa.
4. **Semina** kuhusu Mama Bikira Maria
5. **Hija Pugu**: kwa lengo la kuwaombea na kuwaenzi mababa wamisionari,
6. **Matendo ya huruma:** Hii ilijumuisha kuwapatia waumini wenye shida mbalimbali vyakula na mahitaji kupitia michango mbalimbali na mfuko wa Mt. Vincent.

Parokia pia ina vyama vya kitume kama ifuatavyo;
UWAKA; WAWATA; VIWAWA, UTOTO MTAKATIFU, Mt Vicent wa Paulo, Karismatiki Katoliki, Lejio Maria, UKWAKATA, Moyo Mtakatifu wa Yesu, Watumishi wa Altare, Focolare Movement, Walei Katoliki, Lejio, Wasoma Masomo, Wazee Wastaafu; Parokia Inaundwa na kamati mbalimbali kuanzia Kamati Tendaji Parokia, Katoliki, Lejio Jumuiya Ndogondogo. Parokia inazungukwa na Dini, Madhehebu na Taasisi mbalimbali za serikali na za kijamii.
Mwaka 2025 Agusti kulitokea mabadilishano ya kawaida ya kiuongozi ambapo aliyekuwa Paroko (PD. Emmanuel Bwanamudogo) pamoja na Paroko Msaidizi (PD. Herimenegild Mushi) walihamishwa vituo kupelekwa sehemu mbalimbali. Kutokana na mbadilishano huyo, PD. Dietrich Pendawazima (Paroko wa sasa) na PD. Pierre (Paroko Msaidizi) walihamia katika kituo cha BMC.

Kwa sasa Parokia inahudumiwa na Paroko huyo (PD. Dietrich Pendawazima), Paroko Msaidizi, pamoja na Masista Wateresina wakishirikiana na Masista wa Macapuchini na Kamati Tendaji Halmashauri ya Walei Parokia.

Uongozi wa Parokia ni Kama ifuatavyo:

i. Paroko:

Pd Diedrich Pendawazima IMC (0767029869)

ii. Masista

Sr. Jema [**Mama mkubwa**]: xx
Sr. Leonida: 0765765703

iii. Kamati Tendaji 2026-2029:

a) Peter Mtatiro - Mwenyekiti (**0713 436190**)
b) Evarist Mkandara - Makamu Mwenyekiti (**0758 245133**)
c) Dr. Catherine A. Masao - Katibu (**0758 206780**)
d) Petro Bundara - Katibu Msaidizi (**065 2492323**)
e) George Kakala - Mtunza Hazina (**0656 896558**)

1. RATIBA YA OFISI

SIKU	MUDA ASUBUHI	AINA YA HUDUMA	MUDA JIONI	AINA YA HUDUMA
JUMATATU	02:00—06:00	Ofisi	09:00—11:00	Ofisi
JUMANNE	02:00—06:00	Ofisi	09:00—11:00	Ofisi
JUMATANO	**H A K U N A H U D U M A**			
ALHAMISI	02:00—06:00	Ofisi	10:00 - 11:00 11:00—12:00	Kuabudu binafsi na Kitubio Ibada ya Kuabudu Wote
IJUMAA	12:30	Kutembelea wagonjwa *	09:00—11:00: 11:00 –12:00:	Ofisi Misa na Masifu
JUMAMOSI	02:00– 06:00	Ofisi	10:00 11:00	Ndoa Maungamo

***Utume wa kutembelea wagonjwa ni mara mbili kwa mwezi - Ijumaa ya 1 na ya 3 ya mwezi**

2. RATIBA YA SALA NA IBADA ZA WIKI PAROKIANI

SIKU	MUDA	TUKIO
JUMATATU	12:30 Asubuhi	Misa na Masifu
JUMANNE	12:30 Asubuhi	Misa na Masifu
JUMATANO	12:30 Asubuhi	Misa na Masifu
ALHAMISI	12:30 Asubuhi	Misa na Masifu
	10:00 Jioni	Kuabudu Binafsi & Kitubio
	11:00 Jioni	Kuabudu kwa Pamoja
IJUMAA	12:30 Asubuhi	Kutembelea wagonjwa (Ijumaa ya 1 na ya 3)
	11:00 Jioni	Misa na Masifu
JUMAMOSI	12:30 Asubuhi	Misa na Masifu
JUMAPILI (DOMINIKA)	12:30 Asubuhi	Misa ya 1
	02:30 Asubuhi	Misa ya 2
	04:30 Asubuhi	Misa ya 3 (Watoto)

NB: Huduma ya Kitubio ni kila siku mara baada ya Misa ya asubuhi na Jumamosi ni saa 11 mpaka 12 jioni. Dominika za zaka Hakuna misa ya 3, watoto wanashauriwa kuhudhuria misa ya 2 pamoja na wazazi wao.

3. SALA YA ROZARI TAKATIFU

MWEZI	MUDA	MAHALI
MEI	11:00 Jioni	Parokiani—Grotto
OKTOBA	11:00 Jioni	Parokiani—Grotto

**** Alhamisi Sala ya Rozari itakuwa kabla ya ibada ya kuabudu**

4. RATIBA YA MISA ZA KANDA

(a) MISA ZA MWEZI

KANDA	SIKU
KIVUKONI	Jumamosi ya 2 ya Mwezi
TUAMOYO	Jumamosi ya 2 ya Mwezi
TUNGI	Jumamosi ya Mwisho ya mwezi
KISIWANI	Jumamosi ya Mwisho ya mwezi

5. TARATIBU ZA WAAMINI

(a) Kubariki Nyumba za Waamini

Kubariki nyumba ni kwa Kipindi maalumu , wakati wa Majilio, Kwaresima pamoja na sikukuu ya Somo wa Jumuiya kutegemea na mpango wa ratiba za Parokia na Jumuiya husika.